



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P 950, 411404 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi"; Simu: 255(026)2161200; Barua pepe: ocag@nao.go.tz; Tovuti: www.nao.go.tz

NAIBU SPIKA AFUNGA MAFUNZO KWA WABUNGE YA KUWAONGEZA UJUZI WA KUCHAMBUA NA KUJADILI RIPOTI ZA UKAGUZI

- AAHIDI KUENDELEA KUIMARISHA UHUSIANO WA BUNGE NA OFISI YA CAG
- APONGEZA JITIHADA ZA CAG KUWAELIMISHA WABUNGE KUHUSIANA NA RIPOTI ZA UKAGUZI

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azan Zungu amefunga mafunzo kwa Wabunge yaliyolenga kuwaongeza ujuzi wa kuchambua na kujadili ripoti za ukaguzi zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mafunzo hayo ambayo yamefanyika Mkoani Singida yamewahusisha Wabunge wa Kamati nne (4) za Kudumu za Bunge ambazo ni pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) pamoja na Kamati ya Bajeti.

Naibu Spika ameipongeza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kazi nzuri inayofanya katika kudhibiti na kusimamia matumizi ya fedha za umma ambapo amesema, "Wengi tunatambua kazi nzuri mnayoifanya hasa kwa kuwa jicho la nchi katika kusimamia matumizi ya Serikali na rasilimali za Taifa."

Ameongeza kwamba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina njia bora za kuhakikisha mianya ya rushwa inazibwa kwa kuititia aina mbalimbali za kaguzi zinazofanya. "Ni muhimu kama nchi kupambana na rushwa na kuimarisha maadili ya watumishi wa umma ili wananchi wapate huduma kwa wakati na bila upendeleo, pia napenda kutambua mchango wa Ofisi yenu kwa kuwa kiungo muhimu katika kuimarisha mahusiano ya Mabunge ya ndani na nje ya bara la Afrika kwa kuititia Secretariati ya SADCOPAC ambayo imekuwa chini ya ulezi wa CAG tangu mwaka 2003 hadi leo na kusaidia mahusiano kuimarika," amesema Naibu Spika.

Naibu Spika amemuhakikisha CAG kuwa uhusiano uliopo baina ya Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi utaendelea kuimarishwa kwa maslahi mapana ya Taasisi zote mbili na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Bw. Charles Kichere amelishukuru Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwake katika kutelezeza majukumu yake hususani kwa kuititia Kamati za Bunge ambazo amekuwa akifanya nazo kazi kwa karibu.

“Tunayo msemo kuwa CAG ni jicho la Bunge, katika kuwezesha hilo ni pamoja kufanya kila kinachowezekana kuwajengea uwezo Wabunge na hasa wa Kamati hizi ili waweze kutimiza majukumu yao ya kujadili na kuchambua taarifa hizi kwa tija na ufanisi,” amesema CAG.

CAG, Kichere ametumia nafasi hiyo kuwapongeza Wabunge hao kwa kutenga muda na kushiriki kwenye mafunzo mbali na kuwa na majukumu mengi hasa katika kipindi hiki ambacho Bunge linaendelea na vikao vya Bajeti jijini Dodoma.

Katika hatua mpya CAG amesema kwa sasa anaagalia uwezekano wa kupeleka mafunzo haya katika ngazi ya Mabaraza ya Madiwani. ‘Mpango wangu ni kuanza na Halmashauri za Majiji, kisha Manispaa na baadae Wilaya na Miji, kwani ngazi hii ya utawala nayo ina majukumu makubwa ya kusimamia maendeleo katika maeneo yao ya Kiutawala.

Kwa upande mwingine ameahidi kuongezewa muda wa kutosha wakati wa mafunzo hayo kujadili ripoti za ukaguzi wa ufanisi (**Performance audit**) na pia kuweka kipaumbele katika kujadili ripoti za ukaguzi wa wakati husika (**Real time audit**) ambapo alisema ripoti hizo zikijadiliwa kwa wakati zitaleta tija na mapendekezo ya CAG na Bunge kufanyiwa kazi katika wakati muafaka ikiwemo Kamati hizi kuweza kujadili taarifa za ukaguzi mara tu zinapowasilishwa Bungeni.

Ofisi ya Taaifa ya Ukaguzi huwa ina utaratibu na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwaongeza ujuzi Wabunge wa Kamati za Kudumu za Bunge mara kwa mara ili kuwawezesha katika utendaji kazi wao wa kusimiamia Serikali katika matumizi na kulinda rasilimali za Taifa.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT)

13 Juni, 2022.



Jiandae kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022